# Zana Rahisi Ya Kadi Ya Alama Za Umaskini Tanzania

Mark Schreiner

20 Agosti 2021

Waraka huu na zana ya kukusanya data ziko kwa lugha ya Kiswahili kwenye scorocs.com
This document and a data-collection app are in English at scorocs.com

Zana rahisi ya kutathmini umaskini ya Kadi ya Alama za Umaskini ya Scorocs® (*Scorocs® Simple Poverty Scorecard®-brand poverty-assessment tool*) ni mbinu nafuu, na wazi ya kutumiwa na miradi ya kuwasaidia maskini nchini Uganda ili kuthibitisha na kuboresha utendakazi wao wa kijamii ili kupata kujua washiriki wao vyema zaidi. Majibu kwa maswali 10 ya kadi ya alama yanaweza kutumika:

— Kukagua viwango vya umasikini na idadi ya watu maskini miongoni mwa washiriki wanaojiunga
— Kufuatilia mabadiliko katika umaskini miongoni mwa washiriki waliopo
— Kuainisha washiriki kwa ajili ya kushughulikiwa kwa njia tofauti kulingana na umaskini

## Dokezo la toleo

Kadi hii mpya ya alama ya Tanzania inategemea data za mwaka wa 2018. Inachukua nafasi ya kadi za zamani za alama zilizo kwenye Schreiner (2016 na 2016) ambazo zinategemea data za mwaka wa 2011/12 na za 2007. Kadi hii mpya ya alama inapaswa kutumika kuanzia sasa kuendelea mbele. Makadirio hayawezi kulinganishwa kwenye kadi tatu za alama kwa sababu zinatumia fafanuzi tofauti za *umaskini*. Hivyo basi, makadirio ya mabadiliko katika umaskini baada ya muda ni lazima yatumie kadi sawa ya alama kimsingi na kwa ufuatiliaji.

## Shukrani

Chalice imefadhili hati hii. Data zimetolewa kwenye shirika la Tanzania's National Bureau of Statistics. Shukrani kwa Novati Buberwa, Albina Chuwa, Nadia Belhaj Hassine Belghith, Alisha Lebouthillier, MaryAnne McKinnon, Sylvia Meku, Rose Mungai, na Richard Valliant. Imetafsiriwa na SwahiliSpace.

"Scorocs" and "Simple Poverty Scorecard" are Registered Trademarks (and "Prove and improve the good you do" and "PovIt!" are Trademarks) of Scorocs, L.L.C. for its brand of poverty-assessment tools. Copyright © 2021 Scorocs.

# Scorocs® Simple Poverty Scorecard® Tool

| | | | Jina | Kitambulishi |
|---|---|---|---|---|
| Nambari ya mahojiano: | | | | |
| Tarehe ya mahojiano: | | Mshiriki: | | |
| Nchi: | TZA | Ajenti wa nyanjani: | | |
| Kadi ya alama: | 003 | Kituo cha huduma: | | |
| Sampuli ya uzito: | | | Idadi ya jamaa wa kaya: | |

| Swali | Jibu | Alama |
|---|---|---|
| 1. Kaya yako inaishi katika eneo lipi? (*Kulingana na maarifa ya mhoji*) | A. Ruvuma, au Lindi | 0 |
| | B. Dodoma, Mwanza, Rukwa, au Shinyanga | 4 |
| | C. Tanga, Morogoro, Arusha, au Iringa | 6 |
| | D. Pwani, Geita, Simiyu, Manyara, Njombe, au Katavi | 7 |
| | E. Kigoma, Mtwara, Singida, Tabora, au Songwe | 8 |
| | F. Dar es Salaam, Kagera, Mbeya, Kilimanjaro, au Mara | 12 |
| 2. Kuna jamaa wangapi katika kaya? (*Kulingana na "Lahakazi ya Ukurasa wa Nyuma")* | A. Nane au zaidi | 0 |
| | B. Saba | 5 |
| | C. Sita | 6 |
| | D. Tano | 9 |
| | E. Nne | 13 |
| | F. Tatu | 19 |
| | G. Wawili | 28 |
| | H. Mmoja | 40 |
| 3. Ni nyenzo gani kuu iliyotumiwa kutengeneza sakafu ya nyumba kuu? | A. Udongo/mchanga, samadi, vipande vya vinyl au asphalt, mbao, mnazi/mwanzi, au nyingine | 0 |
| | B. Sementi, tile za kauri, au mbao za parquet au zilizochuliwa | 6 |
| 4. Kaya inamiliki jiko lolote la makaa? | A. La | 0 |
| | B. Ndiyo | 3 |
| 5. Kaya inamiliki meza zozote? | A. La | 0 |
| | B. Ndiyo | 3 |
| 6. Jamaa yeyote wa kaya anamiliki televisheni? | A. La | 0 |
| | B. Ndiyo | 12 |
| 7. Jamaa yeyote wa kaya anamiliki simu ya mkononi? | A. La | 0 |
| | B. Ndiyo | 6 |
| 8. Jamaa yeyote wa kaya anamiliki ng'ombe, mbuzi, kondoo, au nguruwe wowote? | A. La | 0 |
| | B. Ndiyo | 3 |
| 9. Katika juma lililopita, kaya ilikula kuku, mbuzi, samaki, nyama ya ng'ombe, au nyama nyingine yoyote? | A. La | 0 |
| | B. Ndiyo | 7 |
| 10. Kwa kawaida kaya hula milo mingapi kwa siku? | A. Miwili au chache | 0 |
| | B. Tatu au zaidi | 8 |


Copyright © 2021 Scorocs.
**Score:**

## Karatasi ya Kazi ya Ukurasa wa Nyuma: Jamaa wa Kaya

Jaza kichwa cha kadi ya alama kwanza. Jumuisha kitambulishi cha kipekee cha mahojiano (ikiwa kinajulikana), tarehe ya mahojiano, na sampuli ya uzito wa mshiriki (ikiwa unajulikana). Kisha rekodi jina kamili na nambari ya utambulisho ya kipekee ya mshiriki huyo (ambaye huenda akawa ni tofauti na anayejibu), ya ajenti wa nyanjani wa mshiriki (ambaye huenda akawa tofauti na mhoji), na ya kituo cha huduma ambacho mshiriki hutumia (ikiwa kipo na ikiwa kinajulikana). Weka mduara kwenye jibu la swali la kwanza la kadi ya alama ("Kaya  yako inaishi katika eneo lipi?") bila kumuuliza mhojiwa.

Kisha umsomee mhojiwa: *Tafadhali nieleze jina la kwanza (au lakabu) la kila jamaa wa kaya.* Kaya *ni mtu mmoja pekee au kundi la watu (bila kujali uhusiano wa damu au ndoa) ambao kwa kawaida wanagawana matumizi, wanajumuisha rasilimali zao pamoja, na wameishi katika makazi sawa kwa angalau wiki mbili*.

Andika jina la kwanza au jina la utani la kila jamaa, ukianzia na kiongozi na mwanandoa (mkubwa zaidi) wa kiongozi (ikiwa yupo). Onyesha kiongozi na mwanandoa wake (ikiwa yupo) ni yupi. Rekodi idadi ya jamaa wa kaya kwenye kichwa cha kadi ya alama karibu na "Idadi ya jamaa wa kaya:". Then circle the response to the second scorecard question about the number of household members.

Andika jina la kwanza au jina la utani la kila jamaa, ukianzia na kiongozi na mwanandoa (mkubwa zaidi) wa kiongozi (ikiwa yupo). Rekodi idadi ya jamaa wa kaya kwenye kichwa cha kadi ya alama karibu na "Idadi ya jamaa wa kaya:". Kisha uweke mduara kwenye jibu la swali la pili la kadi ya alama linalohusu idadi ya jamaa wa kaya.

Soma maswali yanayofuata kwa sauti. Kila wakati ukumbuke na ufuate maagizo yaliyo kwenye "Mwongozo wa Mahojiano".

| Jina la kwanza au jina la utani? |
|---|
| 1. |
| 2. |
| 3. |
| 4. |
| 5. |
| 6. |
| 7. |
| 8. |
| 9. |
| 10. |
| 11. |
| 12. |
| 13. |
| 14. |
| 15. |
| **Idadi ya jamaa wa kaya:** |

# Mwongozo wa Mahojiano

Marejeleo yaliyonukuliwa hapa yametlewa kwenye:

National Bureau of Statistics. (2017) “Instruction Manual: Household Budget Survey, 2017/18”, [*Mwongozo*].

_____. (2017) “Questionnaire: Household Budget Survey, 2017/18”, [*Hojaji*], link.

## 1. Maagizo msingi ya mahojiano

Kadi ya alama inaweza kujaza kwenye karatasi nyanjani, na majibu kujazwa baadaye kwenye kwenye kompyuta au katika hifadhidata yako binafsi. Vinginevyo, zana ya kukusanya data ya Scorocs iliyo kwenye wingu inafanya kazi vyema katika kivinjari mtandao au kama programu ya simu ya Android, ambayo inawezesha uingizaji data nyanjani au ofisini. Ikiwa hakuna intaneti, basi data inahifadhiwa kwenye kifaa mpaka wakati kutakuwa na intaneti. Pakua zana ya kukusanya data, au uliza kuhusu akaunti ya kibinafsi.

Kadi ya alama inapaswa kuwasilishwa na mhoji aliyepitia mafunzo ya kufuata Mwongozo huu.

Kwanza jaza kichwa cha kadi ya alama na “Karatasi ya Kazi ya Ukurasa wa Nyuma”, ukifuata maelekezo yaliyo kwenye “Karatasi ya Kazi ya Ukurasa wa Nyuma”.

Katika kichwa cha kadi ya alama, jaza idadi ya jamaa wa kaya kulingana na orodha ambayo wewe na mhoji mlitengeneza kama sehemu ya “Karatasi ya Kazi ya Ukurasa wa Nyuma”.

Usiulize swali la kwanza la kadi ya alama wazi wazi (“Kaya  yako inaishi katika eneo lipi?”). Badala yake, jaza jibu kulingana na maarifa yako kuhusu eneo ambapo kaya inaishi.

Kwa njia sawia, usiulize swali la pili la kadi ya alama wazi wazi (“Kuna jamaa wangapi katika kaya?”). Badala yake, weka alama kwenye jibu kulingana na idadi ya jamaa wa kaya ambao uliorodhesha kwenye “Karatasi ya Kazi ya Ukurasa wa Nyuma”.

Muulize mhojiwa moja kwa moja maswali yote nane yaliosalia.

Pitia mwongozo huu kwa uangalifu, na uubebe unapofanya kazi. Fuata maagizo yaliyo katika mwongozo huu (pamoja na agizo hili).

Kumbuka kwamba mhojiwa katika mahojiano haya si lazima awe jamaa wa kaya ambaye anashiriki katika mpango wako.

Vivyo hivyo, ajenti wa nyanjani arekodiwe katika kichwa cha kadi ya alama si lazima awe mhoji kama wewe ambaye anaendesha mahojiano. Badala yake, ajenti wa nyanjani ni mwajiriwa wa mpango wa kuwasaidia maskini ambao mshiriki ana uhusiano nao ambao unaendelea. Hakuna ajenti kama huyo, basi andika “HAKUNA” katika nafasi hizo kwenye kichwa cha kadi ya alama.

Kwa ujumla, usiache nafasi zilizo kwenye kichwa zikiwa tupu. Ikiwa maelezo yanayohitajika hayajulikani, hayapo, au hayawezi kutumika, basi andika “HAKUNA”, “HAIJULIKANI”, “HAIPO”, au “HAITUMIKI” katika nafasi hizo. Hii inaonyesha kwamba wewe kama mhoji ulijaribu kupata data hizo na hivyo inaweza kusaidia kuepuka haja ya kurudi kwa kaya hiyo baadaye ili kujaribu kupata data hizo.

Soma kila swali bila kuruka neno lolote, kwa mpangilio uliowekwa kwenye kadi ya alama.

Unapoweka alama kwenye jibu la swali la kadi ya alama, andika alama kwenye safu ya “Alama” na kisha uweke mduara kwenye jibu la maneno, alama iliyochapwa, na alama za kuandikwa kwa mkono, kama hivi:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3. Ni nyenzo gani kuu iliyotumiwa kutengeneza sakafu ya nyumba kuu? | A. Udongo /mchanga, samadi, vipande vya vinyl au asphalt, mbao, mnazi/mwanzi, au nyingine | 0 | **0** |
| | B. Sementi , tile za kauri, au mbao za parquet au zilizochuliwa | 6 | |

Wakati suala linapoibuka ambalo halijaangaziwa katika Mwongozo huu, suluhu yake inapaswa kutolewa na mhoji na mhojiwa, kwani hiyo ndio kawaida ya UBOS ya Tanzania katika NBS ya mwaka 2018. Yaani, mpango unaotumia kadi hii ya alama haupaswi kutoa ufafanuzi au sheria zozote (isipokuwa zile zilizo katika Mwongozo huu) za kutumiwa na wahoji wake wote. Chochote ambacho hakijaangaziwa moja kwa moja katika Mwongozo huu kiachiwe uamuzi wa kila mhoji na mhojiwa binafsi.

Usimsomee mhojiwa machaguo ya majibu. Badala yake, soma swali, na uachie hapo; subiri jibu. Mhojiwa akiomba ufafanuzi au akisitasita au aonekanae kuchanganyikiwa, soma swali hilo tena na utoe usaidizi kulingana na Mwongozo huu au jinsi wewe kama mhoji unavyoona inafaa.

Kwa ujumla, unapaswa kukubali majibu yanayotolewa na mhojiwa. Hata hivyo, mhojiwa akisema kitu chochote—au ukiona au ukihisi jambo—ambacho kinaashiria kwamba jibu hilo si sahihi, kwa mhojiwa hana uhakika, au kwamba mhojiwa angependa kuopata usaidizi ili kubaini jinsi atajibu, Basi unapaswa kusoma swali tena na kumpa usaidizi unaoona ni mwafaka kulingana na Mwongozo huu.

Ilhali majibu mengi kwa maswali yaliyo katika kadi ya alama yanaweza kuthibitibishwa, mara nyingi hauhitaji kuthibitisha majibu. Unapaswa kuthibitisha tu ikiwa kuna jambo linaashiria kwamba huenda jibu likawa si sahihi na hivyo basi uthibitishaji huenda ukaimarisha ubora wa data. Kwa mfano, unaweza kuchagua kuthibitisha endapo mhojiwa atasitasita, anaonekana kuwa na uwoga, au vinginevyo anaashiria kwamba anadanganya, amechanganyikiwa, au hana uhakika. Vivyo hivyo, uthibitishaji huenda ukawa mwafaka ikiwa mtoto katika kaya inayohojiwa au jirani aseme kitu ambacho hakilingani na jibu la mhojiwa. Pia uthibitishaji ni mzuri ukiona kitu ambacho kinaashiria kwamba jibu si sahihi, kama vile kitu ambacho mhojiwa anasema hamiliki, au mtoto anayekula chumbani ilhali hakuhesabiwa kama jamaa wa kaya hiyo.

Kwa ujumla, matumizi ya kadi ya alama yanapaswa kufanana kwa karibu zaidi kadri iwezekanavyo na matumizi ya HBS ya mwaka 2018 na NBS ya Tanzania. Kwa mfano, mahojiano yanapaswa kufanywa ana kwa ana na mhoji aliyepitia mafunzo katika makazi ya mshiriki kwa sababu HBS ilifanya jambo sawia katika NBS ya mwaka 2018.

# 2. Tafsiri

Kufikia wakati wa uandishi huu, kadi yenyewe ya alama, “Karatasi ya Kazi ya Ukurasa wa Nyuma”, na Mwongozo huu zinapatikana tu kwa lugha za Kiingereza na Kiswahili. Bado hakuna tafsiri rasmi na za kitaalamu za lugha nyingine kuu zinazozungumzwa nchini Tanzania. Watumiaji wanapaswa kutazama scorocs.com ili kuona ni tafisri zipi zimefanywa tangu undishi huu kufanywa. Ikiwa bado hakuna tafsiri rasmi na ya kitaalamu kwa lugha inayotakikana, basi tafadhali wasiliana na Scorocs.

# 3. Mwongozo jumla wa mahojiano kutoka kwenye *Mwongozo*

## 3.1 Kukutana na kaya kwa mara ya kwanza

Kulingana na ukurasa wa 7 wa Mwongozo, “Tabia yako na unavyojiwasilisha ni muhimu sana. Kama mhoji, jukumu lako la kwanza ni kuhakikisha uhusiano mzuri na kaya unayohoji. Mwanzoni mwa mahojiano, wewe na mhojiwa ndio wakati mnaaza tu kujuana. Hisia za kwanza za mhojiwa kukuhusu wewe zitaathiri hali yake ya kuwa tayari kushirikiana nawe. Kuwa wa kirafiki unapojiwasilisha.

“Beba barua na kadi ya kitambulisho inayoonyesha kwamba unafanya kazi na [shirika lako].

“Vaa mavazi ya heshima. Kwa sababu baadhi ya kaya hazina viti, wanawake wanapaswa kuwa na khanga au kitenge cha kuwasaidia wanapoketi.”

## 3.2 Jukumu lako kama mhoji

Kulingana na ukurasa wa 7 na 8 wa Mwongozo, “Wewe kama mhoji unapaswa kuwa ni wewe unaongoza mahojiano. Kama mhoji, jukumu lako ni kukusanya data zinazohitajika. Ubora wa kazi yako unabainishwa na ubora wa data unazokusanya. Kufanikiwa au kutofanikiwa kwa utafiti huu kupo mikononi mwako.

“Kwa uangalifu fuata maagizo yaliyo katika *Mwongozo* huu [pamoja na agizo hili].

“Tengeneza mazingira ya kirafiki ya uaminifu pamoja na mhojiwa ili uweze kupata data sahihi. Ili kufanikisha ili, inasaidia kufahamu utamaduni na tabia za jamii hii.

“Hisia za kwanza unazoleta kutokana na mwonekano wako, maneno yako ya kwanza, na matendo yako ya kwanza ni muhimu sana katika kuhakikisha mhojiwa anashirikiana nawe.

“Waonyeshe wahojiwa kwamba unaelewa unachofanya. Wafahamishe kwamba ushiriki wao unamfaidi [washiriki walio katika mpango wako].

“Usiahidi kaya unayohoji kwamba watapata manufaa ya papo hapo baada ya kushiriki, kwani hii huenda ikapunguza usahihi wa majibu yao.

“Taja kwamba majibu yako yatawekwa faraghani kabisa.

“Usiruhusu watu wengine kuwepo wakati wa mahojiano. Wewe kama mhoji unapaswa kuwa pekee yako pamoja na jamaa wa kaya unayohoji.

“Kuwa fanisi katika kazi yako, lakini usimharakishe mhojiwa.

“Tofauti na mazungumzo ya kawaida, wewe kama mhoji unauliza maswali yote katika mahojiano, naye mhojiwa anakupa majibu yote. Usitoe maoni yako binafsi, na usichangie kwa njia yoyote katika kile ambacho mhoji anasema. Kila wakati usiegemee upande wowote, na usionyeshe kuwa unaunga mkono au hauungi mkono jambo lolote.

“Ikiwa mhoji anasitasita au hayuko tayari kujibu swali, basi jaribu kumshawishi ajibu. Elezea tena kwamba maelezo yote ni ya faraghani. Lakini usisisitize sana; mhoji hawezi kulazimishwa kujibu.

“Fuata kabisa mpangilio wa maswali kama yalivyoandikwa.” Yasome neno kwa neno.

“Chukua usukani wa mahojiano. Dumisha mvutio wa mhojiwa nyakati zote. Mhojiwa akikatisha mazungumzo yetu au akisema mambo bila mpangilio, basi usimdakize mara moja au kwa ujeuri. Sikiliza anachosema, na kisha kwa utaratibu jaribu kumrejesha kwenye swali ulilouliza.”

## 3.3 Faragha

Kulingana na ukurasa wa 4 wa Mwongozo, maelezo unayokusanya “ni ya faraghani kabisa na hayafichuliwi kwa mtu yeyote isipokuwa wale wanaohusika katika utafiti. . . . [Mhakikishie] mhojiwa kwamba maelezo yake yatachukuliwa kwa ufaragha na yatatumiwa kwa madhumuni ya kitakwimu pekee.”

## 3.4 Mhojiwa anapaswa kuwa nani?

Kumbuka kwamba mhojiwa si lazima awe jamaa wa kaya ambaye anashiriki katika mpango wako (ingawa mhojiwa pia anaweza kuwa jamaa huyo).

Kulingana na ukurasa wa 6 wa Mwongozo, “Ikiwa kiongozi wa kaya hayupo, basi jamaa mwingine yeyote wa kaya anaweza kuhojiwa.” Hii inamaanisha kwamba mhojiwa anayependelea ni kiongozi wa kaya.

## 3.5 Kiongozi wa kaya ni nani?

Kumbuka kwamba kiongozi wa kaya anaweza au akakosa kuwa jamaa wa kaya ambaye anashiriki katika mpango wako (ingawa kiongozi pia anaweza kuwa jamaa huyo).

Kulingana na ukurasa wa 13 wa Mwongozo, *kiongozi wa kaya* ni “mtu anayetambuliwa kama kiongozi na jamaa wengine wa kaya. Mara nyingi yeye ndiye anawajibikia usaidizi wa kifedha na maslahi ya jamaa wa kaya.”

# 4. Miongozo ya kila swali katika kadi ya alama

## 4.1 Kaya yako inaishi katika eneo lipi?

A. Ruvuma, au Lindi
B. Dodoma, Mwanza, Rukwa, au Shinyanga
C. Tanga, Morogoro, Arusha, au Iringa
D. Pwani, Geita, Simiyu, Manyara, Njombe, oau Katavi
E. Kigoma, Mtwara, Singida, Tabora, au Songwe
F. Dar es Salaam, Kagera, Mbeya, Kilimanjaro, au Mara

Isipokuwa iwe inabidi, usimuulize mhojiwa swali hili wazi wazi. Badala yake, jaza jibu kulingana na maarifa yako kuhusu eneo ambalo kaya inaishi.

## 4.2 Kuna jamaa wangapi katika kaya?

A. Nane au zaidi
B. Saba
C. Sita
D. Tano
E. Nne
F. Tatu
G. Wawili
H. Mmoja

Usimuulize mhojiwa swali hili wazi wazi. Badala yake, weka alama kwenye jibu kulingana na idadi ya jamaa wa kaya ambao uliorodhesha kwenye "Karatasi ya Kazi ya Ukurasa wa Nyuma".

Kulingana na ukurasa wa 13 wa Mwongozo, *kaya* inajumuisha jamaa ambao wanagawana matumizi na ambao wanakusanya rasilimali zao pamoja.

"Kaya inaweza kujumuisha jamaa mmoja, au zaidi ua jamaa mmoja.

"*Kaya ya mtu mmoja* inajumuisha mtu anayeishi pekee yake, katika sehemu ya makazi au makazi yote, na matumizi ni yake pekee.

"*Kaya ya watu zaidi ya mmoja* ni kundi la watu wawili au zaidi ambao kwa pamoja wanaishi katika sehemu ya makazi aua makazi yote na wanagawana matumizi yao. Aina ya kawaida ya kaya inajumuisha mume, mke, na watoto wao. Jamaa wengine wa familia, waliokodisha makazi, wageni, na watu wengine wanazingatiwa kuwa *jamaa wa kaya inayohojiwa* ikiwa wanaleta rasilimali zao pamoja, wanagawana matumizi, na wameishi na kaya inayohojiwa kwa angalau wiki mbili.

"Wafanyakazi wa nyumbani wanazingatiwa kuwa jamaa wa kaya inayohojiwa iwapo tu wanakula milo yao pamoja na kaya inayohojiwa na wanamtambua kiongozi wa kaya inayohojiwa kama kiongozi wao (bila kujali kana kwamba wafanyakazi hao wa nyumbani wanalala kwenye makazi ya kaya inayohojiwa).

"Watoto wa jamaa wa kaya inayohojiwa ambao wapo katika shule ya bweni wanazingatiwa kuwa jamaa wa kaya inayohojiwa.

"Waliokodisha makazi/bweni/makazi ambao wanalipa kaya inayohojiwa kwa makazi na milo wanazingatiwa kuwa jamaa wa kaya inayohojiwa. Wengine wanaoishi pamoja na kaya inayohojiwa lakini hawashiriki rasilimali na milo pamoja na kaya inayohojiwa hawazingatiwi kuwa jamaa wa kaya inayohojiwa.

“Mwanamume aliye na wake katika zaidi ya kaya moja anapaswa kuzingatiwa kuwa jamaa wa kaya inayohojiwa ikiwa anakaa na kaya inayohojiwa kwa zaidi ya nusu ya muda wake.”

Mtu yeyote ule ni jamaa wa kaya moja (moja pekee). Kaya yoyote ile ina kiongozi mmoja (mmoja pekee). Kiongozi wa kaya yoyote ile ni lazima awe jamaa wa kaya hiyo. Hakuna mtu anaweza kuwa kiongozi wa zaidi ya kaya moja.

Kulingana na Sehemu ya 1 (“Sifa za Mhojiwa”) ya *Hojaji*, *kaya* ni “watu wote ambao kwa kawaida wanaishi [katika makazi pamoja na mshiriki halisi wa mpango wako] na ambao wanakula milo yao pamoja.

Unapojaza “Lahakazi ya Ukurasa wa Nyuma”, rekodi majina ya jamaa wa kaya kwa mpangilio ufuatao:

- “Kiongozi wa kaya
- Mwanandoa/mpenzi wa kiongozi (ikiwa yupo)
- Jamaa wengine wa familia ya karibu (msingi) ya kiongozi ambao kwa kawaida wanaishi [katika makazi pamoja na mshiriki halisi wa mpango wako] na ambao wanakula milo yao pamoja
- Jamaa wengine wa familia au wasio wa familia (kama vile wafanyakazi nyumbani wanaoishi katika makazi) ambao kwa kawaida wanaishi [katika makazi pamoja na mshiriki halisi wa mpango wako] na ambao wanakula milo yao pamoja
- Mtu yeyote mwingine ambaye hayupo sasa katika makazi lakini ambaye kwa kawaida anaishi [katika makazi pamoja na mshiriki halisi wa mpango wako] na ambaye anakula milo yake pamoja”

## 4.3 Ni nyenzo gani kuu iliyotumiwa kutengeneza sakafu ya nyumba kuu?

A. Udongo/mchanga, samadi, vipande vya vinyl au asphalt, mbao, mnazi/mwanzi, au nyingine
B. Sementi, tile za kauri, au mbao za parquet au zilizochuliwa

Kulingana na ukurasa wa 43 wa Mwongozo, wewe kama mhoji unapaswa kumuuliza mhoji swali hili; usiweke alama kwenye jibu kulingana tu na kile ambacho wewe mwenyewe unaona kuhusu sakafu.

Swali hili linahusu sakafu ya nyumba kuu ya makazi ya kaya inayohojiwa.

Rekodi aina ya nyenzo iliyotumika kwenye sehemu kubwa zaidi ya sakafu.

Kulingana na ukurasa wa 14 wa Mwongozo, *makazi* ni “mahali ambapo kaya moja inaishi, bila kujali mpangilio wake. Kwa mfano, makazi yanaweza kuwa chumba kimoja, au inaweza kuwa kitengo kimoja (au zaidi) cha nyumba.”

### 4.4 Kaya inamiliki jiko lolote la makaa?

A. La
B. Ndiyo

Kulingana na ukurasa wa 52 wa Mwongozo, “Usizingatie majiko ya makaa ambayo hayapo kwenye hali nzuri ya kutumika isipokuwa wewe kama mhoji uthibitishe kwamba kaya inatarajia kuyakarabati katika kipindi cha miezi tatu ijayo.

“Majiko ya makaa ambayo kaya ilipokea kama msaada yanapaswa kuzingatiwa.”

## 4.5 Kaya inamiliki meza zozote?

A. La
B. Ndiyo

Kulingana na ukurasa wa 52 wa Mwongozo, “Usizingatie meza ambazo hazipo kwenye hali nzuri ya kutumika isipokuwa wewe kama mhoji uthibitishe kwamba kaya inatarajia kuzikarabati katika kipindi cha miezi tatu ijayo.

“Meza ambazo kaya ilipokea kama msaada zinapaswa kuzingatiwa.”

## 4.6 Jamaa yeyote wa kaya anamiliki televisheni?

A. La
B. Ndiyo

Kulingana na ukurasa wa 52 wa Mwongozo, “Usizingatie televisheni ambazo hazipo kwenye hali nzuri ya kutumika isipokuwa wewe kama mhoji uthibitishe kwamba kaya inatarajia kuzikarabati katika kipindi cha miezi tatu ijayo.

“Televisheni ambazo kaya ilipokea kama msaada zinapaswa kuzingatiwa.”

## 4.7 Jamaa yeyote wa kaya anamiliki simu ya mkononi?

A. La
B. Ndiyo

Kulingana na ukurasa wa 52 wa Mwongozo, “Usizingatie simu za mkononi ambazo hazipo kwenye hali nzuri ya kutumika isipokuwa wewe kama mhoji uthibitishe kwamba kaya inatarajia kuzikarabati katika kipindi cha miezi tatu ijayo.

“Simu za mkononi ambazo kaya ilipokea kama msaada zinapaswa kuzingatiwa.”

## 4.8 Jamaa yeyote wa kaya anamiliki ng'ombe, mbuzi, kondoo, au nguruwe wowote?

A. La
B. Ndiyo

Kulingana na ukurasa wa 70 wa Mwongozo, "Zingatia tu ng'ombe, mbuzi, kondoo, au nguruwe wanaomilikiwa na jamaa wa kaya inayohojiwa. "Usizingatie ng'ombe, mbuzi, kondoo, au nguruwe wanaotunzwa na kaya inayohojiwa lakini wanamilikiwa na kaya nyingine."

### 4.9 Katika juma lililopita, kaya ilikula kuku, mbuzi, samaki, nyama ya ng'ombe, au nyama nyingine yoyote?

A. La
B. Ndiyo

*Mwongozo* hauna maelezo yoyote ya ziada kuhusu swali hili.

## 4.10 Kwa kawaida kaya hula milo mingapi kwa siku?

A. Miwili au chache
B. Tatu au zaidi

Kulingana na ukurasa wa 74 wa Mwongozo, “Swali hili linahusu idadi ya milo ambayo kwa kawaida kaya inayohojiwa hula kwa siku. Hii inajumuisha chamshakinywa, chamchana, na chajio. Hii ni milo iliyotayarishwa na kuliwa nyumbani.”